



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps


© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Kwanza

MUNGU ANAWAITA WATU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Kumbu-kumbu la Torati 6:20-25; 26:16-19

Je, kunayo milima pale unapoishi? Ikiwa ipo, Je! umewahi kuipanda milima hiyo? Je, wewe huona nini uwapo juu ya milima hii? Unaweza kuona vitu vyote vilivyoko chini, misitu, bahari na kila kitu! Kila kitu huonekana kidogo sana. Kila kitu huonekana kama ni sawa.



Pengine uliuona mti mkubwa wa mbuyu ulipokuwa ungali mle bondeni kabla ya kuupanda mlima huo. Au pengine ulisimama na kuliangalia ua zuri nyekundu. Je! Ulikaa kando ya

mtu au kunawa humo miguu yako? Kwa sasa kila kitu ni tofauti kwa sababu umepanda juu ya kilele cha mlima huo. Sasa unakitazama kitu kimoja, lakini sehemu kubwa ya nchi.

Tutaiangalia Biblia katika njia hii, katika masomo matatu yafuatayo. Hatuendi kujifunza juu ya mtu fulani au tusome hadithi fulani. Tunataka tuione Biblia kama kitabu chenye hadithi moja.

**BIBLIA INATWAMBIA JINSI
MUNGU ALIVYOFANYA KAZI
KATI YA WANADAMU**

Biblia ni hadithi ihusuyo jinsi Mungu alivyofanya kazi na mwanadamu ili kumrudisha katika uhusiano mwema naye mwenyewe. Inatwambia jinsi Mungu alivyoumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Inatwambia jinsi mwanadamu alivyotenda dhambi. Tunapata ukweli ulio muhimu sana katika sura tatu za kwanza za Mwanzo na katika sura

tatu za mwisho za Ufunuo. Ukweli huu unaonyesha uhusiano ulioko baina ya Mungu na ulimwengu wake. Tunaona kwamba Mungu aliuumba ulimwengu wote na anatawala kila sehemu yake. Mungu aliuumba ulimwengu mwema. Mungu alimpa mwanadamu uhuru naye akachagua kutenda maovu. Uovu uliingia ulimwenguni kwa sababu ya kuasi kwa mwanadamu na sasa hali ya ulimwengu haiko jinsi Mungu alivyoupangia. Hata hivyo, Mungu yungali anashughulika kumrudisha mwanadamu na ulimwengu kwake. Mwishowe, maovu yote yataangamia na kusudi jema la Mungu litatimizwa.

Biblia ni rekodi ihusuyo jinsi Mungu yuko mbioni kuukomboa ulimwengu.

Mungu hufanya kazi ulimwenguni kupitia kwa watu. Aliwachagua Wayahudi miaka mingi iliyopita. Aliwaita ili wamtii. Alijidhihirisha kwao kwa njia maalum. Aliwaita pia kushiriki uelewaji wao wa Mungu na watu wengine wa ulimwengu. Mungu anawataka watu wote wa ulimwengu kufahamu upendo wake na mpango wake wa ukombozi.

MUNGU ALIFANYA AGANO NA IBRAHIMU



Mungu alipatana au aliagana na mwanadamu ili kufanya kazi pamoja naye. Alifanya agano la kwanza na Nuhu. Halafu akafanya agano lingine na Ibrahimu. Agano ni mapatano kati ya watu wawili. Kulingana na Maandiko neno hili “agano” linaeleza ushirika wa mwanadamu na Mungu.

Mungu alimwita Ibrahimu ili amfuate na kumtii. Mungu alimwambia kwamba angeubariki ulimwengu wote kupitia kwake.

MUNGU ALIMWITA MUSA

Uzao wa Ibrahimu walikuwa watumwa kule Misri baada ya miaka mingi kupita. Mungu alitenda kulingana na historia (alifanya kazi yake hapa ulimwenguni) alipo-waongoza Waisraeli kutoka utumwani. Kiongozi wao alikuwa mtu aitwaye Musa. Mungu alimwambia Musa na watu hao kwamba angewaongoza hadi kwa nchi nzuri ambapo wangekuwa taifa kuu.

Mungu alikuwa mwaminifu katika kutimiza agano lake kwa watu wake. Hata ingawa walitenda dhambi na kumwasi, yeye hakuacha kuwapenda wala kutowaonyesha njia nzuri ya kufuata.

Wana wa Israeli walizunguka jangwani kwa muda wa miaka arobaini wakimgonja Mungu awaruhusu kuingia Nchi ya Ahadi. Ingekuwa nchi ambayo Mwana wa Mungu angezaliwa baada ya miaka mingi kupita.

MUNGU ANAWAPA AMRI WATU WAKE

Mungu alikuwa na mambo mengi ya kuwafundisha Wana wa Israeli



kabla ya kuwakubalia kupata nchi yao wenyewe. Mpango wa ajabu ambao Mungu alikuwa nao kwa watu wake aliowapenda ilikuwa ni kuwapa Amri Kumi. Mungu aliwapa watu wake amri hizi ili ziwasaidie katika agano lake nao. Alijua kwamba walihitaji sheria za kuwaongoza. Sheria au amri hizi zilikuwa mwongozo wa kuwaonyesha watu jinsi ya kuishi. Watu hawa walikuwa na wajibu kwa Mungu. Walikuwa pia na wajibu kwa watu walioishi nao. Amri Kumi hizi zilidhihirisha wajibu wao kwa Mungu na mwanadamu.

Sasa soma Maandiko ya leo (Kumbukumbu la Torati 6:20-25 na 26:16-19) ambayo yanatoa muhtasari wa mapatano ya Mungu na watu wake.

Tutaendelea wiki ijayo na hadithi ihusuyo jinsi Mungu alivyoendelea kuwaendea watu wake.

KAZI YA KUFANYA

Kuna usemi fulani hapa chini uhusuo Biblia. Andika herufi ya S (SAWA) kando ya sentensi zilizo za kweli na herufi ya K (KOSA) kando ya sentensi zisizo za kweli.

- Biblia inaschemu mbili, nazo ni Agano la Kale na Agano Jipya.
- Ujumbe wa Agano la Kale na Agano Jipya hauhusiani hata kidogo.
- Biblia ni rekodi jinsi Mungu afanyavyo kazi ya kuukomboa ulimwengu.
- Amri Kumi ni mwongozo wa kutuonyesha jinsi ya kuishi.



Andika katika nafasi ifuatayo elezo lako mwenyewe la Biblia. _____

Andika elezo la neno "agano".

Kunayo maneno magumu katika
somo hili. Jifunze maana ya maneno
yafuatayo:

Waebrania.....Hili ni jina lingine la
Wayahudi; jila la
lugha ya Kiyahudi

Israeli.....Taifa la Wayahudi, jina
lingine la Yakobo.

Agano..... Agano ni mapatano.
Kulingana na jamii,
agano hufanywa baina
ya watu wawili. Ku-
lingana na Maandiko,
agano linaeleza
ushirika wa mwana-
damu na Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**“...Naye Bwana amekuungama
hivi leo kuwa taifa iliyotengwa
iwe yake yeye, kama alivyo-
kuahidi, na kuwa yakupata
kushika maagizo yake yote...”
(Kumbukumbu la Torati 26:18).**

Mungu alipoagana na Israeli
aliahidi kuwabariki na kuwatumia
kwa kuubariki ulimwengu wote.
Aliwapa amri ili waweze kuwa na
mwongozo wa kuwaonyesha jinsi ya
kuishi. Mara kwa mara Waisraeli
walikosa kutii na kuvunja amri hizi,
lakini Mungu hakuwaacha kamwe.
Agano lake lilikuwa agano la neema.
Mungu alimtuma Yesu wakati watu
walipotumia vibaya sheria na kuifanya
kuwa ya muhimu kuliko watu. Yesu
hakuja kuitangua sheria bali
kuitimiza. Alikuwa kuwakomboa watu
kutoka katika dhambi zao.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Pili

MUNGU ANAWAONGOZA WATU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia 31:31-34

Wiki iliyopita tuliachia hadithi ya wana wa Israeli wakiwa jangwani. Mungu alikuwa amewatoa utumwani kule Misri. Aliwafanya Waisraeli kuwa jamii walipokuwa jangwani. Walijua kwamba Mungu alikuwa pamoja nao akiwaongoza, lakini walikosa kutii mara nyingi.

Miaka hii waliyokuwa jangwani ilikuwa migumu sana kwao. Ilikuwa pia migumu kwa Musa. Musa alikuwa mvumilivu sana kwa watu hawa. Kila mara walikuwa wakiasi na bila kuwa na shukrani. Walimlaumu Musa mara kwa mara.

Hitaji kuu ambalo watu walikuwa nalo ni lile la kupata maji. Siku moja watu hao waligombana sana wakati walipokuwa hawana maji. Wali-mlaumu Musa kwa kuwatoa Misri. Mungu alimwambia Musa kwamba akinena na jabali (mwamba) maji yatapatikana. Lakini Musa alikuwa amekasirishwa sana na watu hao.

Badala ya kusema na jabali lile, alilipiga mara mbili kwa fimbo yake. Naye Mungu hakumruhusu kuingia ndani kwa sababu alikosa kumtii.

Kizazi chote cha Waisraeli walifika jangwani. Mwishowe Musa na vijana waliobakia walifika katika nchi ya Moabu. Musa alipanda juu ya mlima Nebo na akaiangalia Nchi ya Ahadi. Alijua kwamba hangeruhusiwa kuingia humo pamoja na wengine na kuitwaa. Hata hivyo, agano hili lingekuwepo hata ikiwa kizazi chote kingekufa. Mungu alitimiza ahadi yake hata ingawa alipaswa kuwachagua viongozi wapya.

WATU WA MUNGU KATIKA NCHI YA AHADI

Mtu aitwaye Yoshua, aliwaongoza Waisraeli hadi kwa Nchi ya Ahadi. Nchi ya Kanaani ilishindwa na ikagawanywa kati ya makabila ya Israeli. Mungu aliwaongoza watu hao akitumia watu waitwao "waamuzi". Mungu ndiye aliyewachagua watu hawa. Hawakuchaguliwa kwa kupiga

kura. Hawakutoka katika jamaa za kifalme. Lakini, uwezo mkuu wa Mungu ulionekana maishani mwao. Watu waliwafuata viongozi hawa walipotambua kwamba wanao uwezo wa Mungu.

Katika wakati huu, watu hawajifunza kwamba walikuwa wakibarikiwa waliposhirikiana pamoja kumtumikia Mungu na kufanya mapenzi ya kulingana na agano. Lakini waliteseka walipomwasi Mungu na kutotii agano lao naye.

ISRAELI INATAKA MFALME

Samweli alikuwa mwamuzi wa mwisho. Alikuwa mtu mkuu sana. Watu walimwambia Samweli kwamba wanataka mfalme. Samweli aliwaambia juu ya hatari ya kuwa na mfalme. Hata hivyo, watu walitaka kuwa taifa lenye nguvu, na walitaka mfalme ambaye angewaongoza katika vita. Sauli alikuwa mfalme wa kwanza wa Israeli.

Mungu alitaka kuwaondolea wana wake mateso ambayo wangeyapata iwapo walifuata mtindo huu. Hali ukweli mkuu wa maisha hauwezi kujifunzwa katika njia nyingine yote. Ni kupita tu kwa matatizo mengi mengi ambayo yangewapata Waisraeli ndipo wangeweza kujifunza juu ya neema na hukumu ya Mungu.

Jamii hii, ya Waisraeli, ikawa taifa. Lilikuwa taifa tajiri na lililojulikana sana chini ya uongozi wa Mfalme Daudi. Lilizidi kuwa tajiri sana chini ya uongozi wa Sulemani, mwanawe Daudi. Lakini watu hao hawa-kutosheka na mwishowe ufalme huo

mmoja uligawanyika katika falme mbili, ya kaskazini na kusini.

Katika mwaka wa 722 B.C. ufalme wa kaskazini uliangamizwa na Waashuru. Nao Ufalme wa kusini uliangamizwa na Wababeli mnamo mwaka wa 587 B.C. Watu hao walishikwa mateka.

MUNGU ANANENA KUPITIA KWA MANABII

Katika wakati huu wa shida Mungu aliwaita watu wa kunena na watu wake, Israeli. Watu hawa waliitwa manabii. Walijaribu kuwaonyesha watu maana na sababu ya shida wanazozipata. Waliwaonya watu kuhusu matokeo ya matendo yao maovu. Manabii hawa walitabiri juu ya kuharibiwa kwa mji wa Yerusalemu na hekalu.

Maandiko ya somo hili yaliandikwa na nabii Yeria. (Yeria 31:31-34) Watu walikuwa huru kuchagua jinsi ya kutenda, lakini hawakuwa huru kuepuka matokeo ya dhambi zao. Taifa hilo liliangamizwa. Watu nao walishikwa mateka na Babeli. Lakini Mungu alikuwa pamoja nao. Angezidi tu kuwaongoza. Angefanya nao AGANO JIPYA.

Watu hao wote hawakuwa pamoja. Baadhi yao walibaki Yuda. Wengine walikimbilia Misri. Wengi wao walishikwa mateka na wakapelekwa Babeli. Manabii wa wakati huu wa kuishi utumwani hawakuamini kwamba Mungu angewaacha watu wake. Ujumbe wao ulikuwa kwamba Mungu ataendelea kufanya kazi ya watu wake.

KAZI YA KUFANYA

Hapo chini kuna picha za watu ambao wametajwa katika somo hili la leo. Chini ya picha hizo kuna usemi uhusuo watu hao. Andika jina la mtu yule kando ya sentensi inayoelezea habari zake.



MUSA



DAUDI



YEREMIAH



YOSHUA



SAMWELI

—Aliwaongoza Waisraeli kutoka Misri hadi Nchi ya Ahadi.

—Aliwaongoza Waisraeli kuingia katika Nchi ya Ahadi.

—Alikuwa mwamuzi wa mwisho wa Israeli.

—Alikuwa mmojawapo wa wafalme wakuu wa Israeli.

—Alikuwa nabii ambaye aliandika Maandiko ya Biblia ya somo letu la leo.

Jifunze maana ya maneno haya.

Waamuzi - Hawa walikuwa wazee waliochukua uongozi wakati Waisraeli walipovamia au kutishwa na majeshi ya nchi zingine walipoishi Palestina.

Mateka - Huu ulikuwa wakati wa kuishi utumwani wakati Wayahudi walioshindwa (wapatao elfu hamsini) walishikwa na kwenda kuishi Ashuru na Babeli. Kipindi hiki kilichukua muda wa miaka hamsini lakini Waebrania wengi hawakurudi kwao.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Bali agano hili ndilo nitakalo-fanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu” (Yeremia 31:33).

Manabii wa Agano la Kale walizungumzia mara kwa mara kuhusu agano ambalo Mungu alikuwa amefanya na watu wake. Yeremia, katika kifungu cha 31 amesema kwamba ataagana upya na watu wake. Agano hili lingandikwa katika mioyo yao. Agano hili linganzia kwa msamaha na ushirika wa mtu na Mungu. Lingekuwa agano la neema. Baada ya miaka mia sita kupita tangu Yeremia aliposema maneno haya, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba, “Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.” (Marko 14:24). Alikuwa anatimiza ahadi ya kale iliyotolewa kwa Yeremia - sasa kulikuwepo na Agano Jipya.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Tatu

MUNGU ANAWAOKOA WATU WAKE


MASOMO YA BIBLIA: Isaya 53:3-6,
Mathayo 28:16-20

**WAISRAELI WANARUDI
KUTOKA UTUMWANI**

Hebu tuendeleo na hadithi yetu ihusuyo jinsi Mungu alivyoshirikiana kikazi na watu wake, Israeli. Waisraeli walishindwa na Babeli. Watu wengi walishikwa mateka na kupelekwa uhamishoni. Hata hivyo, Mungu ambaye alikuwa amewatoa watu wake kutoka Misri alikuwa tayari kutenda jambo lingine la "ajabu". Alinena na watu waliokuwa utumwani kupitia kwa nabii Isaya.

Isaya alitangaza "Habari Njema" ya kuja kwa ukombozi wa Mungu. Alisema kwamba Mungu ange-wawezesha Waisraeli kurudi nchini kwao. Naye Mungu atawatumia kutimiza mpango wake wa ulimwengu.

Nebukadneza, Mfalme wa Babeli alikufa. Muda si muda mtu aitwaye Koreshi aliishinda Babeli. Koreshi



aliwaruhusu baadhi ya watu wa Israeli kurudi Yerusalemu. Watu walijenga tena kuta za Yerusalemu chini ya uongozi wa Nehemia na Ezra. Walijenga pia Hekalu. Ezra alifika akiwa na sehemu ya kitabu cha sheria na akakisoma mbele ya watu. Watu walisikitika sana matendo yao. Walielewa kwamba kushikwa kwao kulikuwa kama hukumu ya Mungu kwao kwa ajili ya kutotii kwao. Hawakuwa wametii sehemu yao ya agano. Waliahidi kuonyesha imani na shukrani zao kwa kutii sheria.

ISAYA ANAIKUMBUSHA ISRAELI KUHUSU MWITO WA MUNGU

Ni huzuni kubwa kwamba baada tu ya miaka michache kupita watu walifanya “kutii sheria” kuwa muhimu zaidi kuliko ushirika wao na Mungu. Walianza kufikiri kwamba wao ni bora zaidi kuliko watu wengine. Walisahau kwamba Mungu alikuwa amewaita ili washiriki imani yao na wengine. Nabii Isaya aliieleza Israeli kuwa ni “mtumishi” aliyeitwa kuutumiza mpango wa Mungu. (Isaya 53:3-6) Lakini Israeli walishindwa na wakashikwa mateka. Nabii huyu anaendelea kusema kwamba Mungu atawatumia watu wachache watakaobakia ili kutimiza kazi yake. Hawa wachache ni wale waliorudi kutoka uhamishoni. Lakini hata hao walishindwa walipoifanya sheria kuwa ya muhimu sana. Walipoteza ufahamu wa kazi ambayo Mungu aliwataka wafanye. Isaya alikuwa amesema kwamba Israeli ilipaswa iwe “nuru kwa watu wa Mataifa”. Hii inamaanisha kwamba ilipaswa kushiriki ufahamu wake wa Mungu na watu wengine. Israeli ilipaswa iwe mtumishi ambaye mateso yake yatawafaidi wanadamu wote. Lakini Israeli ilipoteza uwezo wa kuona mwito wake.

YESU NDIYE MTUMISHI ATAKAYETESWA

Mwishowe, nabii huyu anatumia neno “mtumishi” kuzungumza juu ya mtu atakayeokoa watu wa Mungu. Maneno yaliyoko katika Isaya 53:3-6 yanaeleza kazi ya Yesu Kristo miaka mingi kabla ya kuja kwake.



Baada ya miaka mingi kupita Rumi iliitoka Yerusalemu. Maandiko ya Agano Jipya yanaeleza hadithi ya yale yaliyotokea. Yohana Mbatizaji, nabii wa mwisho wa Kiebrania, alifika na akasema kwamba “siku ya hukumu” i karibu”. Malaika walitangaza “Habari Njema” ya kuja kwa Kristo.

Injili ya Agano Jipya inazungumzia kuhusu “Habari Njema” hii. Agano Jipya inazungumzia kuhusu Injili ya Habari Njema ya wokovu wa Mungu, jinsi Isaya alivyokuwa amesema kuhusu kuja kwa wokovu wa Mungu. Mungu alikuwa amefanya “tendo lingine la ajabu”. Tendo hili la Mungu lilibadili historia yote. Liko katikati ya imani ya Mkristo. Ni kilele cha kujifunua kwa Mungu kwa mwanadamu. Yesu Kristo ndiye Habari Njema. Amekuja kuwaokoa wanadamu na kuwapa maisha mapya.

Katika kitabu cha Kutoka Mungu aliwatoa watu wake kutoka utumwani. Hili lilikuwa tendo la ajabu la Mungu. Kutolewa kwa Wayahudi kutoka utumwani kule Babeli ilikuwa kazi ya Mungu. Sasa Mungu amefanya kazi iliyokuu kushinda zote. Alimtuma Yesu aishi, afe na afufuke. Wanadamu wanaweza kuwa na ushirikiano mpya wao kwa wao kupitia kwa Kristo.

KRISTO HULIANZISHA KANISA

Yesu aliwaita wale wanafunzi kumi na wawili. Mwujiza mkuu ulifanyika wakati watu hawa walipoelewa maana ya maisha, kufa na kufufuka kwa Yesu. Jamii hii ndogo ilikuwa kanisa. Jamii hii haikupaswa iwe ya watu wachache tu, lakini ilikuwa kwa watu wote, iwapo ni Myahudi au Mtu wa Mataifa. Mtu ye yote anaweza kuwa sehemu ya jamii hii, yaani kanisa, iwapo ataamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu kwamba damu yake ilimwagika kwa ajili ya dhambi zake na akubali kwa imani kufa na kufufuka kwa Yesu na amkubali Kristo awe Bwana wa maisha yake. Jamii hii, kanisa, ndipo Israeli mpya. Ni jamii ya Agano Jipya.

Agano Jipya inatwambia kuhusu kazi ya Yesu Kristo katika uanzilishaji wa kanisa. Inatwambia pia, jinsi kanisa lilivyoenea katika sehemu mbali mbali za ulimwengu wa siku hizo.

Vifungu hivi vya Mathayo 28:16-20 vinatwambia jinsi Yesu alivyolipa kanisa kazi ya kufanya. Soma vifungu hivi. Je! kazi hii ni ipi? Ni kushiriki Habari Njema ya Yesu Kristo na ulimwengu wote.

Je! unaelewa ni kwa nini sehemu ya kwanza ya Biblia inaitwa Agano la Kale hali sehemu ya pili inaitwa Agano Jipya? Hata hivyo, kumbuka kwamba ilimpasa Mungu kuagana upya na watu wake, abao alikuwa tu na mpango mmoja nao. Kuna ujumbe mmoja mkuu katika Biblia ambao unaunganisha pamoja Agano la Kale na Agano Jipya. Biblia inazungumzia kuhusu upendo na jinsi Mungu anavyojishughulisha na mwanadamu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mwishowe, Mungu alishihirisha mpango wake wa kumwokoia Mwanadamu.

Kwa hivyo, utaona kwamba kulikuwa tu na mpango mmoja hata ingawa ilimpasa Mungu kuagana upya na watu wake. Mpango huo ulikuwa wa kumrudisha mwanadamu kuweza kushirikiana na Mungu kupitia kwa Yesu Kristo, Yesu hakuja kuanzisha mpango mwingine. Yesu amesema katika Mathayo 5:17 kwamba, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza."

Biblia inatwambia jinsi Mungu alivyofanya kazi katika maisha ya wanadamu ili kumkomboa kila mwanadamu. Mungu yungali anafanya kazi ulimwenguni kupitia kwa kanisa lake. Kitabu cha mwisho cha Biblia, UFUNUO, kinasema kwamba hakuna awezaye kushinda kusudi la Mungu. Ushindi ni wake.

KAZI YA KUFANYA

Katika masomo matatu yaliyopita tumejifunza jinsi Mungu alivyo-shirikiana kikazi na mwanadamu, jinsi ilivyoandikwa katika Biblia.

Hapo chini kuna sentensi ambazo zinatwambia baadhi ya mambo ambayo Mungu alifanya. Orodha ya mambo haya haijafuatana vizuri. Andika namba kando yake kulingana na jinsi yalivyofanyika.

—Mungu aliwapa Waisraeli Amri Kumi kupitia kwa mtu aitwaye Musa.

—Mungu alimwita mtu aitwaye Ibrahimu na akafanya agano naye. Alimwambia kuondoka katika nchi yake na kwenda katika nchi ambayo atamwonyesha.

—Mungu aliwaonya watu juu ya matendo yao maovu kupitia kwa watu waitwao manabii.

—Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi kwa Nchi ya Ahadi, Kanaani.

—Mungu alifanya agano jipya na watu wake. Alimtuma Mwana-we, Yesu, kuja ulimwenguni ili awaokoe wanadamu kutoka katika dhambi zao kuwarudisha katika ushirika wa haki naye.

—Mungu aliwatoa Waisraeli kutoka uhamishoni (utumwa) kule Babeli.

—Yesu Kristo alianzisha kanisa ili kueneza Habari Njema kwa ulimwengu wote.

Baadhi ya watu hawaelewi nabii ni nani. Jifunze maelezo yafuatayo.

Nabii - Neno "Nabii" katika lugha ya Kiebrania linamaanisha yule anayezungumza kwa niaba ya mwingine. Nabii wa Kiebrania

aliwaambia watu ujumbe wa Mungu. Wakati mwingine alitoa ujumbe wa matumaini akielezea yale ambayo Mungu atafanya wakati ujao. Nabii alikuwa mtu ambaye alijisikia kuwa ameitwa na Mungu kuhubiri na kuzungumza kwa ujasiri badala yake.

Injili - Neno hili "injili" linamaanisha "habari njema". Mafundisho na maisha yake Yesu, hasa kifo chake, kukiwa, na kufufuka, ni injili ya Kristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6).

Mungu amekuwa akijishughulisha katika kumrudisha mwanadamu awe na ushirika mwema naye tangu wakati mwanadamu alipofanya dhambi na kumwasi. Mwishowe alimtuma Yesu ulimwenguni ili atufie ndipo tusamehewe dhambi zetu.

Kila mmoja wetu amefanya dhambi. Yesu Kristo amefia kila mmoja wetu. Je! unashukuru kwa ajili ya zawadi hii kubwa ya wokovu? Ikiwa unashukuru, basi utaonyesha shukrani zako kulingana na jinsi unavyoishi. Utamkubali kwa imani, na uwe sehemu ya kanisa lake na ufanye kazi ya kuwaambia wengine yale ambayo Kristo amekufanyia.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU . KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Nne

MPENDE MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:3; Mathayo 4:8-10; Marko 12:28-30

AMRI YA KWANZA

Mungu anataka awe wa kwanza katika mioyo na maisha ya watu wake. Mungu ndiye aliyetuumba. Anataka kuwa na ushirika nasi. Anatupenda na atatutaka nasi tumpende.

Hapo kale Mungu aliwaambia Waebrania kwamba, "Usiwe na miungu mingine ila mimi" (Kutoka 20:3). Hii ndiyo iliyokuwa amri ya kwanza kati ya zile Amri Kumi ambazo Mungu alimpatia Musa kwenye Mlima Sinai.

Je! unadhani kwamba watu wa Mungu walikuwa wakitii amri hii? La, hashu. Watu hawa walisahau mara kwa mara amri hii. Baadhi yao waliabudu sanamu zilizotengenezwa kwa dhahabu au mawe. Wakati

mmoja walimwabudu mungu aitwaye, Baali. Mungu naye akawatuma mmojawapo wa manabii kwao. Nabii huyu alitwa Eliya. Eliya aliwakemea sana watu hao. Je! mtaendelea (kujaribu kuwatumikia miungu wawili hadi lini)? "Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! mfuateni yeye" (1 Wafalme 18:21).

Eliya alijua kwamba Baali hakuwa Mungu. Baali alikuwa tu sanamu. Mungu ni wa kweli, Mungu aishiye anayewapenda watu wake na kuwasaidia. Mungu tu wa kweli, aishiye ndiye awezaye kupenda.

Kunaye Mungu mmoja tu wa kweli. Hakuna Mungu wa Wahindi, wa Waafrika na wa Wazungu. Kuna Mungu mmoja tu. Naye ni Mkuu. Yeye ni mtakatifu na mwenye haki. Ni mwenye uwezo wote. Yeye ni Mungu mwenye upendo na ni yeye pekee anayestahili upendo wetu.

MUNGU ANAWAPENDA WATU WAKE

Tunajua kwamba Mungu amekuwa akiwapenda watu ambao aliwaumba kwa sababu tunayo rekodi ya upendo wa Mungu kwa watu wake katika Biblia. Mwanadamu alifanya dhambi. Alikosa kumtii Mungu, lakini Mungu hakuacha kumpenda. Mungu alinena na mwanadamu kupitia kwa watu kama Ibrahimu, Musa, Eliya na manabii wengine wote, lakini mwanadamu aliendelea tu kutomtii Mungu. Kutotii huku kulikuwa kama ukuta kati ya Mungu na mwanadamu. Ulizua kutokuwa na ushirika kati yao. Lakini Mungu alimpenda sana mwanadamu hata akajaribu kwa njia nyingi kuondoa ule ukuta ulio-watenganisha. Mwishowe Mungu alikuja ulimwenguni kupitia kwa Yesu Kristo. Yesu anatuonyesha jinsi Mungu alivyo. Anatuonyesha kwamba Mungu ni upendo. Alitufia ili ule ukuta wa dhambi na kutotii uondolewe. Sasa twaweza kufahamu upendo wa Mungu iwapo tutaupokea.

YESU ALITII NA AKAFUNDISHA AMRI YA KWANZA

Hata Yesu alijaribiwa kufuata njia ya kibinafsi. Ibilisi alimjaribu Yesu alipokuwa nyikani. Alimwonyesha Yesu falme zote za ulimwengu. Halafu akamwambia, "Haya, yote nitakupa, ukianguka kunisujudia" (Mathayo 4:8-10).

Yesu alimjibu Ibilisi. Akamwambia, "Nenda zako Shetani; kwa maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake."

Siku moja, mtu mmoja alimwendea Yesu na akamwuliza kwamba ni amri ipi iliyo ya kwanza na kuu kuliko zote. Yesu akamkariria kifungu kutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, akamwambia, "Ya kwanza ndiyo hii, sikia Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote" (Marko 12:28-30).

JE! UNAMPENDA MUNGU?


Mungu anawataka watu wake wampende sana yeye kila wakati. Je! tunampenda Mungu kwa mioyo yetu yote, na kwa roho zetu zote na kwa akili zetu zote? Je! tunampenda kuliko mtu au kitu kingine cho chote?

Tunapompenda Mungu, huwa tunamfanya Bwana wa maisha yetu. Hutaka kumtumikia na kuishi kwa ajili yake kila siku. Huwa tunamtumikia Mungu wakati tunapomtii. Tutamtii iwapo tunampenda.

Huwa hatuwezi kutii sheria zile zingine iwapo hatumpendi Mungu kuliko mtu au kitu kingine cho chote. Huwa hatuwezi kuishi maisha ya haki bila msaada wa Mungu. Tunaweza tu kupata uwezo na nguvu za kushinda majaribu na dhambi iwapo tutamruhusu Mungu aishi maisha yake ndani yetu. Tutapata ushindi maishani mwetu wakati roho wake anapotuongoza.

KAZI YA KUFANYA

Hapa kuna picha ya mbao za mawe inayofanana na ile iliyoandikwa zile Amri Kumi. Andika amri ya kwanza kwenye picha hii. (Tazama Kutoka 20:3).



Kuna maneno ambayo yameachwa katika aya ifuatayo. Utapata maneno na picha inayoelezea katika orodha iliyoko chini ya sentensi hizi. Jaza nafasi iliyoachwa kwa neno lililosahihi.

Mungu aliwataka watu wake wampende sana kila wakati, lakini hawakufanya hivyo wakati wote. Wakati mmoja waliabudu _____ mkubwa aitwaye Baali. Hata siku hizi kunao watu wengine ambao wanapenda sana mali na vitu vingine kuliko Mungu. Baadhi ya watu wanapenda sana _____ kuliko kitu kingine. Au wanaweza

kufikiri kwamba utajiri unaopatikana kwa kuwa na _____ ni wa muhimu sana. Watu wengine hufanya _____ kuwa ya kwanza maishani mwao. Watu wengine hufikiria kwanza vitu kama _____ nzuri. Wengi hufanya nafsi yao kuwa ya kwanza, wakitaka tu kujifurahisha bila kuwafikiria wenzao.



Ng'ombe



pesa



sanamu



gari



elimu

Mwandishi mmoja alimwendea Yesu na akamwuliza ni amri ipi iliyo ya kwanza kwa zote. Yesu alimjibu kwa kumwambia maneno yaliyoko katika kifungu cha kukumbuka cha leo. Amri hii ndiyo msingi wa amri zingine zote. Hatuwezi kuwapenda wenzetu iwapo hatumfanyi Mungu kuwa wa kwanza na pia kumpenda sana. Hatuwezi kuishi jinsi inavyotupasa iwapo hatutii amri hii ya kwanza.

Utataka kumtii Mungu iwapo unampenda. Andika katika nafasi ifuatayo njia mojawapo ambayo utajaribu kumtii Mungu kwayo wiki hii ijayo. _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja, nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote" (Marko 12:29-30).



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Tano

MUNGU ANATAKA IBADA YA KWELI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:4-6; Yohana 4:7-10, 19-24

JE! IBADA NI NINI?

Je! unapoinamisha kichwa chako kabla ya kula, huwa unamshukuru Mungu kweli kwa ajili ya chakula hicho? Je! umewahi kuona haragwe liotalo likitokezea udongoni na ukamshukuru Mungu kwa ajili ya jua na mvua iliyolisaidia kukua? Je! umewahi kusikiliza jinsi moyo wako

unavyopiga na ukamshukuru Mungu kwa uhai ulionao? Ikiwa umeshukuru, basi umemwabudu Mungu kwa moyo wa kweli.

Soma Kutoka 20:4-6. Tunapata amri ya pili kati ya zile Amri Kumi katika vifungu hivi. Tumeamriwa kumwabudu tu Mungu wa kweli. Amri ya pili ni hii, "Usijifanyie sanamu ya kuchonga."

Baadhi ya watu husema kwamba sanamu au mifano huwasaidia kumfikiria Mungu. Biblia inasema kwamba, "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" (Yohana 4:24). Hatupaswi kuwa na sanamu ya kutusaidia kumfikiria Mungu. Hatuhitaji sanamu yakutusaidia kumwabudu Mungu.

Je! ibada ni nini? Unapomwambia Mungu "asante", huwa unamwabudu. Unapoimba wimbo wa kumsifu Mungu huwa unamwabudu.



Wakati mwingine watu huinamisha vichwa vyao wakati wa kuomba au hufungua midomo yao na kuimba, lakini wanajifanya tu kuwa wanaabudu. Wanaenda kanisani lakini mioyo yao iko mbali sana na Mungu. Hata ingawa watu hawa wanafuata utaratibu wote wa Ibada, huwa hawamwabudu Mungu hata kidogo.

Kila mtu hapa ulimwenguni ana ile hamu ya kumjua Mungu. Sote tunadai kuwa na urafiki na Mungu. Lakini hatuwezi kusimama mbele za Mungu jinsi tulivyo kwa sababu Mungu ni mtakatifu. Sote tumefanya dhambi. Yesu, Mwana wa Mungu hakufanya dhambi yote. Alikufa ili kuchukua adhabu tuliyostahili. Mara tu unapomwamini Kristo, huwa umezaliwa katika jamaa ya Mungu. Nawe huwa mtoto wake. Hata unaweza kusimama mbele za Mungu na kumwabudu kwa ajili ya yote aliyokufanyia. Mungu anawatafuta wavulana na wasichana ambao watamwabudu kwa kweli na kwa mioyo yao yote.

Hata hivyo, ibada ni zaidi ya kushukuru na kusifu kwa nyimbo. Ikiwa tunampenda kweli Mungu, basi tutaishi maisha ambayo yatampendeza. Huwa tunamwabudu Mungu kwa matendo yetu na mawazo yetu. Ikiwa yale tunayofanya kila siku na kufikiria hayampendezi Mungu, basi maombi na nyimbo zetu havifai kitu.

NI LINI NA NI WAPI UWEZAPO KUABUDU

Je, unaweza kuabudu lini? Unaweza kuabudu wakati wo wote na mahali po pote katika jengo la kanisa,

nyumbani, unapofanya kazi, au unaposoma. Wakristo hukutanika kuabudu katika siku maalumu iitwayo Jumapili. Tunapaswa pia kumwabudu Mungu kila siku po pote tulipo.

Mungu ni roho. Hatuwezi kuona roho. Je! sasa tunajuaje kwamba Mungu yuko? Tunaona vitu vya ajabu alivyoumba. Unaweza kumtengeneza mtu kutoka kwa udongo, lakini huwezi ukampulizia pumzi ya uhai. Mungu tu ndiye awezaye kumwumba mwanadamu.

Ikiwa wewe ni Mkristo, unajua kwamba Mungu yuko kwa sababu ya yale aliyokufanyia maishani mwako. Yeye ndiye anayestahili sifa na ibada zako.



Yesu alizungumza na mwanamke Msamaria aliyekuja kisimani kuchota maji. Alikuwa amechoka na alihitaji kupumzika. Yesu alimwambia kuhusu maji ya uzima. Aliyafananisha na uzima wa milele ambao hupatikana tu kwa Mungu. Alipomwambia kwamba baba zake waliabudu milimani, Yesu alimdhahirisha wazi kwamba haijalishi pale ambapo mtu anafanyia ibada. Ni hali ya moyo wake iliyo ya muhimu. Mungu anawatafuta wale wanao-

abudu kwa kweli, sio watu ambao hufuata tu utaratibu wa kwenda kanisani au kuomba. Soma hadithi ya mwanamke Msamaria katika Yohana 4.

Je! Mungu anaona nini kwako? Je! unaabudu kwa moyo wa kweli? Mwambie Mungu kuhusu jambo hili. Mwombe akusaidie ili umwabudu kwa moyo wa kweli.

KAZI YA KUFANYA

Kuna sentensi hapo chini. Baadhi yao yanaelezea matendo ya ibada ya kweli, na mengine hayaelezei. Andika neno NDIYO kando ya sentensi yaelezayo ibada ya kweli na uandike LA kando ya yale sentensi mengine.

- 1. Nazitazama nyota na na kusema, “Mungu ni wa ajabu. Aliumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Hali yungali na muda wa kuni-sikiliza.”
- 2. Kuna sanamu moja ya mwanadamu kwenye meza pale ukutani. Mtu mmoja huisujudia na kuweka chakula karibu nayo.
- 3. Samweli hufunga macho yake wakati mchungaji anapoomba, lakini huwa anafikiria mchezo wa mpira aliocheza wiki iliyopita.
- 4. Mariamu huwa anasema kwa haraka sala alilokariri, kabla ya kulala na kuitikia “Amina”, halafu anachukua kitabu cha hadithi na kuanza kukisoma.

- 5. Wanjiru humwangalia mtoto na kusema, “Ona jinsi mtoto huyu alivyomzuri! Hebu viangalie vidole vyake. Ni ajabu ilioje jinsi Mungu alivyofanya muumbo wa kupendeza?”

Taja mahali patatu ambapo unaweza kumfanyia Mungu ibada ya kweli.

1. _____
2. _____
3. _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Mungu ni roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli” (Yohana 4:24).

Tunapomwabudu Mungu tunapaswa kukumbuka yale aliyo sema Yesu. Mungu ni roho. Yuko kila mahali. Hatuwezi kumwona, lakini yu pamoja nasi tunapoabudu. Tunaweza kumwabudu Mungu wakati wo wote na mahali po pote kwa sababu yeye ni roho. Ibada yetu huwa inakubaliwa iwapo yale tunayosema na kufanya wakati wa ibada ni ya kweli.

Hatupaswi kutumia sanamu wakati wa ibada kwa sababu Mungu ni roho. Biblia inatuambia kwamba Mungu yu ndani yetu iwapo sisi ni Wakristo. “Hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?” (1 Wakorintho 6:19). Mungu yu nasi kila mara kwa sababu anaishi ndani yetu. Kwa nini tuhitaji msaada wa sanamu ili tumfikirie Mungu? Jambo hili halimpendezi Mungu.

“Njoni, tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele zake kwa shukrani, tumfanyie shangwe kwa zaburi. Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, na Mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mikononi mwake zimo bonde za dunia, hata vilele vya milima ni vyake. Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya, na mikono yake iliumba nchi kavu. Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba. Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, Na kondoo za mkono wake”

Zaburi 95:1-7a.

Hii ni zaburi ya kuabudu. Pengine utataka kujifunza kwa moyo.





VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Sita

UWE MWAMINIFU KATIKA IBADA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:7; Mathayo 5:33-37; Marko 7:5-8 .

UMUHIMU WA JINA

Je! unaitwa nani? Je! jina lako lina maana fulani? Majina ni ya muhimu sana. Wazazi huwa waangalifu sana wanapochagua majina ya watoto wao. Majina yanaweza kumwelezea mtu au jamaa. Jina la mtu huchukua mahali pa mtu mwenyewe.

Leo tutajifunza amri ya tatu. Inatwambia ni lazima tuheshimu jina la Mungu. Nayo inasema kwamba, "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako." (Kutoka 20:7)

Waisraeli waliogopa na waliheshimu sana jina na utu wa Mungu. Wengi wao hawakutaja jina la Mungu. Hawakutaja jina la Mungu kwa sababu walimweshimu sana. Mungu ni mtakatifu. Kwa hivyo, jina lake ni takatifu kwa kuwa yeye ni mtakatifu.

Tunapaswa kutumia jina la Mungu kwa uangalifu tunapoomba na

kuabudu. Tunakutumia tu jina la Mungu tunapo mtukuza. Amri ya tatu inatwambia kwamba ni kosa kulitaja bure jina la Mungu au kulifanyia mzaha.

YESU ANAFUNDISHA KUHUSU AMRI YA TATU

Siku moja Yesu alizungumzia kuhusu amri ya tatu mbele ya umati wa watu uliokusanyika kando ya mlima. Soma juu ya mazungumzo yake katika Mathayo 5:33-37.

Yesu akawaambia, "Usiape kabisa." Je! wewe huapa? Je! kuapa ni nini? Kuapa ni kutaja jina la Baba Aliye



mbinguni au jina la Mwanawe, Yesu, wakati ambapo hutaki kamwe kuzungumza na Mungu.

Ni kosa kulitaja jina la Mungu ili kusisitiza yale tusemayo. Huwa tunafanya hivyo wakati tusemapo, "Haki ya Mungu, nilisahau," au "Mungu anajua tunasema ukweli." Hatupaswi kutumia neno la Mungu tunapoapa au kulaani. Jina la Mungu ni takatifu jinsi yeye mwenyewe alivyomtakatifu.

NJIA ZINGINE ZA KULITAJA BURE JINA LA MUNGU

Maana ya amri ya tatu ni zaidi ya yale tunayo sema tu. Inamaanisha pia jinsi tunavyoishi. Iwapo tunasema kwamba tunamjua Mungu, lakini tunaishi kama hatumjui, basi tunaivunja amri hii.



Waandishi na Mafarisayo walimjia Yesu wakiwa na malalamiko. "Mbona wanafunzi wako wanakula chakula kabla ya kunawa mikono yao?" Wakamwuliza. "Hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee." (Marko 7:5-8)

Je! ni vizuri kunawa kabla ya kula chakula? Ndiyo! Lakini si dhambi iwapo utasahau kunawa mikono. Yesu alijua mawazo ya mioyo yao na akawaambia, "Imeandikwa, 'Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami.'" (Marko 7:6) Yesu aliwaita wanafiki. Mafarisayo walijifanya kuwa wanampenda Mungu, lakini mioyo yao ilikuwa mbali sana naye.

Kuna hadithi nyingine katika kitabu cha LUKA ihusuyo Mfarisayo na mtoza ushuru. Mfarisayo hakufanya ibada ya kweli kwa sababu alimshukuru Mungu kwa kuwa



alikuwa mwema na si kama yule mtoza ushuru. Alikuwa hasa mnafiki. Mtoza ushuru alisema tu kwamba, "Mungu unirehemu, mimi ni mwenye dhambi!"

Hebu itazame picha ya watu hawa wawili. Pengine utataka kuwachora kwa rangi tofauti iwapo una zile kalamu za rangi.

Mnafiki ni yule anayejifanya tu kuwa vile ambavyo hatendi. Ni kama yule mchezaji afanyaye tu mchezo wa



kuigiza. Katika Tito 1:16 tunapata picha inayomwelezea mnafiki. "Wanafikiri ya kwamba wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao wanamkana; ni wenye machukizo, waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai."

Je! unajifanya kuwa unamfahamu Mungu? Wewe hutendaje uwapo shuleni? Wewe hutendaje ukiwa nyumbani? Huwa unatendaje unapocheza au unapofanya kazi? Ikiwa unasema unampenda Mungu, Je! huwa unaonyesha kwa matendo yako? Au huwa unakosa kutii amri hii ya tatu kwa kulitaja bure jina la Mungu?

KAZI YA KUFANYA

Maneno yafuatayo yametolewa katika Maandiko ya Biblia ya somo la leo. Wameacha nje baadhi ya maneno. Jaza nafasi zilizoachwa kwa kutumia maneno yaliyoko upande wa kushoto. Chagua neno ambalo litakamilisha vyema kila sentensi.

- | | |
|-------------|--|
| huniheshimu | 1. "Lakini mimi nawaambia, _____ kabisa." |
| jina | 2. "Nao _____ bure." |
| maneno | 3. "Bali _____ yenu yawe 'ndiyo' au 'siyo'." |
| amri | 4. "Usilitaje bure _____ la Bwana, Mungu wako." |
| waniabudu | 5. "Watu hawa _____ kwa midomo yao, ila _____ yao iko mbali nami." |
| mapokeo | |
| usiape | 6. "Ninyi mwaiacha _____ ya Mungu na kuyashika _____ ya wanadamu." |
| mioyo | |

Hebu jifikirie wewe mwenyewe, Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika "Ndiyo" au "La".

Je! huwa unasema kwa mdomo wako kwamba, "Nampenda Mungu"? _____

Je! huwa unasema maneno haya kwa moyo wa kweli? _____

Je! huwa unasoma na kuisikiliza
Biblia? _____

Je! matendo yako huwa yana-
dhihirisha maneno usemayo? _____

Je! huwa unamwomba Mungu
akusaidie uishi maisha ya
kumpenda? _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**“Na kwa nini mnaniita, Bwana,
Bwana, walakini hamyatendi
nisemayo?” (Luka 6:46).**

Kusema tu Bwana, Bwana,
hakumaanishi cho chote iwapo
hatumfuati Mungu daima. Siku hizi
watu wengi wanaweza kusema
kwamba, “Ndiyo, naamini Mungu.”
Hali maisha yao yanaonyesha
kwamba hawamjali Mungu kamwe.
Kutenda hivi ni sawa na kulitaja bure
jina la Mungu.

Wafuasi wa Yesu waliitwa Wakristo
kwa sababu walikuwa kama Kristo.
Huwa tunaabudu bure jina la Mungu
iwapo hatuishi jinsi alivyotuagiza
tuishi.



VIJANA TUFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Saba

MATUMIZI MEMA YA SABATO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:8-11; Luka 6:6-11

KUSUDI LA JUMAPILI

Je! siku iitwayo Jumapili ina maana gani kwako? Je! ni siku tofauti na zile zingine? Amri ya nne inasema kwamba, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase." (Kutoka 20:8)

Kulingana na Agano la Kale, siku ya sabato ilikuwa Jumamosi, siku ya saba ya wiki. Wayahudi wote ambao hawakuwa wamemwamini Kristo walikuwa wangali waitunza jumamosi kuwa siku ya sabato.

Yesu alifufuka kutoka kwa wafu wakati wa siku ya kwanza ya wiki, Jumapili. Wakristo walianza kuita Jumapili, "Siku ya Bwana" baada ya Yesu kupaa mbinguni.

Wakristo wameendelea kukutana kwa ajili ya ibada wakati wa Siku ya Bwana, Jumapili. Mungu ametuamuru tuitakase siku hii. Tunapaswa kuwa

waaminifu katika kuhudhuria ibada za kanisa letu. Tulipewa siku hii ili tuweze kutafuta msaada wa mahitaji ya roho zetu.

Siku ya sabato inapaswa pia kuwa siku ya kupumzika kufanya kazi zetu za kila siku. Tulipewa ili iwe siku ya kupumzika na kuisaidia miili na akili zetu. Mungu hakukusudia kwamba tukae tu bila kufanya kitu cho chote.

Kunazo kazi ambazo zinapaswa kufanywa hata Jumapili. Ni lazima tupike na tuitunze jamaa yetu. Watu wengine kama madaktari na wauguzi, wana kazi ambazo ni lazima wafanye siku ya Jumapili. Mungu anaelewa jambo hili.

Hata hivyo, tunapaswa kuifanya Jumapili kuwa siku ya kupumzisha miili yetu jinsi tuwezavyo. Je! Jamaa yako hungojea kwenda sokoni wakati wa Jumapili badala ya Jumamosi?



Huwa unasema kwamba, “Leo siwezi kwenda kuabudu pamoja na Wakristo wengine kwa sababu mama yangu ananitaka niende naye sokoni.” Tunapaswa kufanya matayarisho ya Jumapili wakati wa Jumamosi.

UNAWEZAJE KUITAKASA SIKU YA SABATO?

Tunaweza kupata msaada wa jinsi ya kuitakasa siku ya sabato tukifuata mfano na mafundisho ya Yesu.

Wayahudi walikuwa na sheria nyingi zihusuzo sabato wakati Yesu alipoishi duniani. Kulikuwepo na zaidi ya mambo elfu moja ambayo hawangeweza kufanya wakati wa siku ya sabato. Walikuwa waangalifu kuhakikisha kwamba kila mmoja alitii sheria hizi. Wale ambao hawakutii sheria za siku ya sabato waliadhibiwa vikali.

Wakati Yesu alipokuja, alilaani njia zao za kuitakasa siku ya sabato. Yesu alienda katika Sinagogi wakati mmoja



wa siku ya sabato. Alisimama ili afundishe na akamwona mtu mmoja mwenye mkono uliopooza, yaani, ulikuwa umepindika na hata haufai. Waandishi na Mafarisayo walingojea tu waone kitakachofanyika. Je! Yesu angeponya wakati wa siku ya sabato? Angeweza, na hata aliponya! Watu hao walimwangalia Yesu na macho ya hasira. Yesu alikuwa ametenda mema wakati wa siku ya sabato, hali wao walizidi kumlaumu. Mioyo yao ilikuwa imejaa chuki na mauaji. Soma hadithi hii katika Luka 6:6-11.

Mawazo ya Yesu yameelezwa katika kifungu chetu cha kukumbuka. “...Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia.” (Marko 2:27-28)

Hatupaswi kufanya yale ambayo hayamtukuzi Mungu. Ikiwa Kristo ni Bwana wa maisha yetu, atakuwa pia Bwana wa sabato yetu.

KAZI YA KUFANYA

Baadhi ya maneno yameachwa katika sentensi zifuatazo. Jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno yaliyosahihi.



1. Musa alipewa Amri Kumi na Mungu kwa ajili ya watu wa kale na wa sasa. Amri hizi zinapatikana katika kitabu cha _____, sura ya _____.
2. Amri ya kwanza inasema kwamba, "Usiwe na _____ mingine ila mimi."
3. Amri ya pili inasema kwamba, "Usijifanyie sanamu ya _____."
4. Amri ya tatu inasema kwamba, "Usilitaje bure _____ la Bwana, Mungu wako."
5. Amri ya nne inasema kwamba, "Ikumbuke _____ ya _____ uitakase."

Hapa chini kuna mchezo unaofanana na fumbo. Hii ni picha ya mtu. Unganisha kila namba jinsi zinavyofuatana kwa kuchora mstari ukianza na namba 1. Utakapomaliza utapata picha ya mtu. Je! mtu huyu ni nani?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato" (Marko 2:27).

Yesu alikuwa akiwaambia Mafarisayo kwamba sabato ilitolewa kwa ajili yetu. Hatuhitaji sheria nyingi ili tuitakase siku ya Bwana. Tunapaswa kujifunza neno la Mungu, tuzungumzane naye, na tuabudu na kuomba pamoja na Wakristo wengine. Tunapaswa kupumzisha akili na miili yetu. Tunapaswa kuwatendea wenzetu mema.





VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Nane

WAHESHIMU WAZAZI WAKO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:12; Marko 7:9-13; Luka 2:51-52

MPANGO WA MUNGU KWA JAMAA

Je! unafikiria kwamba ni muhimu kuwatii wazazi wako? Utapata jibu la swali hili baada ya kusoma amri ya tano. Amri hii inasema kwamba, "Waheshimuni baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" (Kutoka 20:12).

Tunaposoma Biblia twaona kwamba Mungu alikuwa na mpango wa kuwepo kwa jamaa. Aliwapangia watoto kuwa na wazazi ambao wangewatunza, na kuwafundisha, na kuwaongoza. Pia, mpango wa Mungu ni kuwataka watoto wawatii wazazi wao. Baba aliye mbinguni anajua njia nzuri ya kuwawezesha watoto wakue na kuwa watu wazima wenye furaha.

Baadhi yenu mnaishi katika miji mikubwa. Pengine kuna wavulana na wasichana katika shule yako ambao wanafikiria kwamba ni "vizuri" kutokuwa mtiifu. Pengine wanafikiri kwamba wazazi wao hawajui kitu kwa sababu hawajasoma.

Kumbuka kwamba wazazi wanafahamu mengi zaidi kuliko wewe kuhusu jinsi ya kuishi hata ingawa hawajasoma. Wanajua matokeo ya kutokuwa mtiifu.

Amri hii ina ahadi kwa watu wa Mungu. Inatwambia kwamba siku zetu zitakuwa nyingi katika nchi tuliyopewa na Bwana iwapo tutawaheshimu wazazi wetu. Mungu alikuwa akiwaambia Wana wa Israeli. Alikuwa akiwaonyesha njia ya kuwa na taifa imara na kuendelea kutenda mema katika nchi ambayo walikuwa wamepewa na Mungu.

Jamaa ambayo watoto wake wanapenda, na kuheshimu, na kuwatii wazazi wao huwa jamaa imara. Taifa linapaswa kuwa na jamaa imara ili liendeleo kuwa taifa lenye nguvu. Matatizo huwa katika kila taifa wakati jamaa yake huanza kuwa dhaifu.

YESU ALISEMAJE KUHUSU AMRI HII YA TANO?

Yesu alifikiriaje amri hii ya tano? Mafarisayo waliwalaumu wanafunzi wa Yesu kwa sababu wakati mwingine hawakuosha mikono yao kabla ya kula chakula. Yesu aliwaambia kwamba wao walikuwa na hatia yakosa kubwa zaidi ya hilo. Wengi wao hawakutaka kuwasaidia wazazi wao waliozeeka. Walisingizia kwamba zawadi ambazo wangewapa wazazi wao, walikuwa wamezitenga kama zawadi za kumtolea Mungu. Hazingetumiwa kwa kuwasaidia wazazi wenye mahitaji. Kwa kweli, Mafarisayo hawa walikuwa wakidanganya ili kukwepa wajibu wao wa kuwasaidia wazazi wao. Soma vifungu hivi vya Marko 7:9-13.

Yesu alikuwa mtiifu wakati alipokuwa mtoto. Watu wazima walisafiri kila mwaka kwenda Yerusalemu ili kuhudhuria sherehe za Pasaka. Yesu alienda pamoja na wazazi wake alipotimiza umri wa miaka kumi na miwili. Baada ya kumaliza sherehe hiyo kundi hilo lilianza safari ya kurudi kwao, Nazareti. Walisafiri muda wa siku nzima kabla ya kutambua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao. Siku tatu baadaye, Mariamu na Yusufu walimpata Yesu akiwa hekaluni huku

akizungumza na walimu kuhusu Mungu. Mariamu alimwita naye akamfuata bila kulalamika. Alikuwa chini ya mamlaka ya Mariamu na Yusufu. Hii inamaanisha kwamba aliwatii. Mungu anakwambia leo kwamba, “Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki.” (Waefeso 6:1)



KAZI YA KUFANYA

Wakati mwingine ni vigumu kuwatii wazazi wako, lakini amri ya tano inatwambia, “Waheshimu baba yako na mama yako.” Njia nzuri ya kuwaheshimu ni kuwatii.

Weka alama ya “X” kando ya kila picha iwapo utajaribu kuiheshimu wakati huu.




Umemaliza chakula chako na umechoka sana. Mama yako anakwambia, "Nenda ukaoshe sufuria."



Unaporudi nyumbani kutoka shuleni pamoja na vijana wengine. Wao wanatumia na kuzungumza maneno mabaya. Naye baba amekwambia, "Usiseme maneno mabaya hata ingawa vijana wenzako watakuchokoza."



Ni siku nzuri ya kucheza na rafiki zako. Baba yako anakwambia, "Mwanangu, leo ni wakati wako kuchunga mbuzi."



Mama amekuacha uwatunze watoto wakati aendapo sokoni. Rafiki yako anakwita ili mwende kucheza, lakini unakumbuka jinsi mama alivyo-kwambia, "Usimwache mtoto peke yake."

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**“Enyi watoto watiini wazazi wenu
katika Bwana, maana hii ndiyo
haki” (Waeefeso 6:1).**

Kuwaheshimu wazazi wetu
inamaanisha kuwatii na kuwasaidia.
Mungu anampango kwa jamaa nā
anawataka watoto wawatii wazazi
wao.

Je! umtiifu kiasi gani? Je! wazazi
wako wanapokwambia kitu, huwa
unawatii mara moja, au hungojea
warudie mara nyingi? Je! uwapo peke
yako na kujaribiwa kutenda jambo
ovu huwa unajiambia, “Wazazi wangu
hawatagundua kamwe,” au, huwa
unakumbuka mafundisho na kuyatii?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Tisa

KUCHUKIA NI DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:13; Mathayo 5:21-24, 43-44; 1 Yohana 3:15-18; 4:20-21

MAUAJI HUANZA MOYONI

Sheria ya Mungu ambayo tunataka tujifunze wiki hii inasema, "Usiue" (Kutoka 20:13). Biblia inazungumzia juu ya kumwua mtu mwingine. Haimaanishi kwamba hatupaswi kuwua wanyama, ndege au samaki na kuwala.

Hakuna aliye na haki ya kumwua mwingine. Uhai hutoka kwa Mungu. Mungu tu ndiye awezaye kupeana uhai. Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Anayo roho. Wakati mtu anapomwua mwenzake huwa anaiangamiza roho ambayo Mungu alimpa.

Pengine unafikiria kwamba watoto hawapaswi kujifunza juu ya amri hii. Ni watoto wachache tu ambao watafikiria juu ya kumwua mwingine. Pengine hii ni kweli. Hata hivyo,

mauaji (kumwua mtu mwingine) hutokana na wivu, hasira, chuki au tamaa ya kujichukulia nafasi ya kwanza. Huanzia moyoni mwa mtu.

Yesu alizungumzia juu ya Amri Kumi za Mungu wakati alipofundisha. Aliwaambia watu kwamba sio mauaji tu ambayo ni tendo baya, bali ni kosa



pia kuwa na chuki. Ikiwa mtu ataenda kumwabudu Mungu, na akumbuke kwamba kunaye yule anayemchukia au ana neno juu yake, basi mtu yule anapaswa kwanza kwenda na kupatana na mwenzake kabla ya kuabudu. Soma Mathayo 5:21-24.

Wakati mwingine hatuwezi kujizuia kukasirika wakati tunapokosewa na mwenzetu. Huwa tunakasirika iwapo mtu si 'mpole kwetu. Yesu amesema kwamba hatupaswi kubakia na hasira zetu. Ni lazima tusamehe.

Petro alimwuliza Yesu kwamba ni mara ngapi ambapo anapaswa kumsamehe mtu ambaye amemkosea. Yesu akamwambia, "Saba mara sabini." Hii inamaanisha kwamba msamaha wetu hauna kikomo.

WAPENDENI ADUI ZENU

Hapo kale watu walifikiria kwamba wanapaswa kuwapenda jirani zao na kuwachukia adui zao. Lakini Yesu alisema kwamba, "Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi" (Mathayo 5:44). Je! ni nani awezaye kufanya hivi? Hakuna awezaye kumpenda adui yake bila kusaidiwa na Mungu. Mtu ye yote anaweza kumpenda adui yake kwa kusaidiwa na Mungu. (Mathayo 5:43-44)

Tunafahamu kwamba ni kosa kumwua mtu mwingine. Neno la Mungu linasema kwamba yule anayemchukia ndugu yake ni mwuaji.

Twajuaje kwamba Mungu anatupenda? Thibitisho ni kwamba alimtuma Mwanawe kufa kwa ajili yetu. Iwapo Mungu anatupenda jinsi


hiyo, nasi tunapaswa kumpenda kwa kiasi ambacho tunaweza kutoa maisha yetu kwa ajili yake. Upendo na chuki haviwezi kuwa katika moyo mmoja wakati mmoja.


Tunaonyeshaje upendo huu? Kwa matendo yetu au jinsi tunavyoishi. "Mtu akisema, 'Nampenda Mungu', naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo." (1 Yohana 4:20a). Soma 1 Yohana 3:15-18 na 4:20-21.

Je! unamchukia ndugu yako, dada yako au mtu mwingine? Basi wewe humpendi Mungu. Mwombe Mungu akuonyeshe picha ya moyo wako. Je! kunayo chuki yo yote? Iwapo iko, basi mwombe Mungu aiondoe. Mwombe aujaze moyo wako na upendo wake.

KAZI YA KUFANYA

Andika jina lako chini ya picha inayoonyesha moyo wako.





Maneno yaliyoko upande wa kushoto hayajakamilika. Chora mstari kutoka kwa maneno yaliyo upande wa kushoto hata kwa yale yaliyoko upande wa kulia ambayo yata-kamilisha maneno haya.

- | | |
|--|--|
| 1. Ninajua Mungu ana-nipenda | Ikiwa unampenda Mungu, mpende pia ndugu yako. |
| 2. Naweza je kumpenda Mungu ambaye sija-mwona? | Nampenda Mungu, huku anamchukia ndugu yake. |
| 3. Mtu ni mwongo iwapo atasema | kwa sababu Mwanawe alitoa maisha yake kwa ajili yangu. |
| 4. Amri mpya ya Mungu inasema, | iwapo siwezi kumpenda ndugu yangu ambaye nimemwona. |

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji; nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake" (1 Yohana 3:15).

Mwandishi wa kifungu hiki anasema kwamba chuki na mauaji ni kitu kimoja. Maneno haya yanaweza kuonekana kama niyakukemea, lakini Yesu hakusema tu kwamba ...yule anayeua atahukumiwa, bali alisema pia kwamba mtu ye yote anaye-mchukia ndugu yake atapata hukumu. (Mathayo 5:21-22)

Biblia inasema kwamba dhambi huleta huzuni na mauti, lakini Mungu anatupa uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo. (Warumi 6:23) Yesu ndiye Mwokozi. Hutusamehe dhambi zetu na kuziondoa tunapomwamini. Hutupa uzima ambao utaishi milele.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Kumi

YESU ANAWASAMEHE WENYE DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:14; Mathayo 5:27-28; Yohana 8:3-11


MPANGO WA MUNGU KWA JAMAA

Si mpango wa Mungu kwamba kila mtu aoe, au aolewe. Lakini Mungu ana mpango kwa yule anayetaka kuoa au kuolewa.

Mungu anasema katika amri ya saba kwamba, "Usizini" (Kutoka 20:14). Hii ni njia ya kusema kwamba unapooa, huwa unaahidi kumpenda na kuwa mwaminifu kwa mtu mmoja hadi wakati ambapo mtatenganishwa na kifo.

Je! ni lazima watu watende kulingana na ahadi hii? Ndiyo, kwa sababu Mungu ndiye aliyepangia kuwepo kwa maisha ya jamii. Mungu alimwumba mtu wa kwanza, Adamu. Mungu akasema, "Si vyema huyo mtu

awe peke yake." Halafu Mungu akamwumba mwanamke wa kwanza, Hawa. Akawaambia wazae watoto. Wao walianzisha jamaa ya kwanza. Nia ya mume na mke, na watoto wao kupendana na kuishi pamoja kwa furaha ilikuwa katika mpango wa Mungu.



Baadhi ya watu hujiondolea furaha kwa kutoishi kulingana na mpango wa Mungu wa kuwa na jamaa yenye furaha. Huvunja ndoa yao kwa kusahau ahadi yao ya ndoa.

Au wanaweza kuoa wake zaidi ya mmoja. Mpango wa Mungu ni kwa mume mmoja kumwoa mke mmoja hadi watakapotenganishwa na kifo.

Wewe jinsi ulivyo ungali kijana sasa wa kuweza kuoa au kuolewa. Lakini wewe si kijana sana wa kuweza kujiamulia kwamba unataka kufuata mpango wa Mungu baadaye ili uwe na ndoa yenye furaha iwapo amekupangia kuoa au kuolewa.

Yesu alisema kwamba tunaweza kuwa na hatia ya kuzini kulingana na vile tunavyojisikia miyoni mwetu kuhusu mtu mwingine. Uzinzi huanzia kwa tamaa mbaya iliyoko akilini na miyoni mwetu. Soma Mathayo 5:27-28.

YESU ALIMSAMEHE MWANAMKE MWENYE DHAMBI

Kulingana na hadithi ya leo, waandishi na Mafarisayo walimletea Yesu mwanamke ambaye alikuwa amevunja ahadi yake ya ndoa. "Tutafanyaje?" Wakamwuliza Yesu. "Je! tumwue kwa kumpiga na mawe?"

Yesu aliinamisha kichwa chake na akaanza kuandika mchangani. Mwishowe akawaambia, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe" (Yohana 8:7). Je! ni mwandishi au Mfarisayo yupi ambaye hakuwa na dhambi hata moja? Hapakuwa na ye yote. Kila mmoja wao alikuwa

amefanya dhambi, jinsi mtu ye yote mwingine aliyezaliwa. Mioyo yao ilikuwa yenye dhambi kama ya kuiba, uongo, uovu na chuki. Hapakuwa na ye yote kati yao ambaye hakuwa na hatia. Je! ni nani aliyetupa jiwe la kwanza? Hapakuwa na ye yote. Dhamira yao iliwaambia kwamba, "Huwezi kumtupia mawe. Hata wewe umefanya dhambi." Kwa hivyo, yule aliyekuwa mzee kati yao aliondoka kimyakimya. Mwingine alimfuata, na hata mwingine pia. Yesu aliinua kichwa chake. Alimwona tu yule mwanamke akiwa peke yake. Yesu alijua kwamba alikuwa amesikitikia dhambi zake. Akamwambia, "Wako wapi wale washtaki wako? Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia?"

"Hakuna Bwana," akamjibu.

"Wala mimi sikuhukumu," Yesu akamwambia. "Enenda zako, wala usitende dhambi tena."

Mwanamke huyu alikuwa amesahau ahadi yake ya ndoa. Hii ilikuwa dhambi kwake. Yesu alimsamehe, lakini ingekuwa vizuri iwapo hakuwa ametenda kwanza dhambi hiyo.



Ishi kulingana na Neno la Mungu. Mwombe Mungu akusaidie kuchagua rafiki wa maisha afaaye. Mwoe Mkristo. Mpende kila mara rafiki yako Mkristo uliyemwoa. Mungu atawapatia furaha. Njia yake ni kuwa mwaminifu katika ndoa!

KAZI YA KUFANYA

Je! umewahi kuandika ujumbe kwa kutumia mpango wa herufi? Utapata hapo chini maneno ya kifungu cha kukumbuka cha leo ambayo yameandikwa kwa kutumia namba. Jaribu kuyatambua ni yapi, halafu uandike neno linalofaa katika nafasi iliyoachwa.

Mpango huu wa herufi ni:

A = 1	J = 10	S = 19
B = 2	K = 11	T = 20
C = 3	L = 12	U = 21
D = 4	M = 13	V = 22
E = 5	N = 14	W = 23
F = 6	O = 15	X = 24
G = 7	P = 16	Y = 25
H = 8	Q = 17	Z = 26
I = 9	R = 18	

Yesu anasema katika Biblia kwamba, "Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya 11-23-5-12-9 _____, yo yote yaliyo ya 19-20-1-8-1 _____, yo yote yaliyo ya 8-1-11-9 _____, yo yote yaliyo ya 19-1-6-9 _____, yo yote yenye 11-21-16-5-14-4-5-26-1 _____, yo yote yenye 19-9-6-1 _____ njema; ukiwapo 23-5-13-1 _____ wo wote, ikiwapo 19-9-6-1 14-26-21-18-9 _____ yo yote, yatafakarini hayo" (Wafilipi 4:8).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo" (Wafilipi 4:8).

Yesu alipozungumza kuhusu amri ya saba alisema kwamba ni dhambi hata kufikiria mawazo mabaya akilini mwako. Alisema hivi kwa sababu wakati mtu ANAPOFIKIRIA mawazo mabaya kwa muda mrefu, huanza kutenda kulingana na fikira zake.

Je! unawezaje kujizuia kutofikiria mawazo mabaya? Neno la Mungu linatupa siri moja katika kifungu cha kukumbuka cha leo. Je! siri hiyo ni ipi?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Kumi na Moja

KUIBA NI DHAMBI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:15; Luka 19:1-10; Marko 12:38-40; Amosi 8:4-5

JE! WIZI NI NINI?

Je! ni vibaya kuiba, au ni vibaya tu kushikwa wakati unapoiba? Mungu anasema kwamba, "Usiibe" (Kutoka 20:15). Mungu hasemi kwamba, "Usiibe vitu vikubwa vikubwa, lakini iba tu vile vidogo." Wala hasemi kwamba, "Hakikisha kwamba hushikwi wakati unapoiba." Anasema tu wazi kwamba "Usiibe." Kuiba ni dhambi.

Je! wizi ni nini? Kuiba inamaanisha kuchukua kitu ambacho si chako. Kunaweza kuwa na vitu ambavyo ni vya jamaa yote. Pengine unaweza kuruhusiwa na wazazi wako kula ndizi usikiapo njaa iwapo kuna mgomba wa ndizi katika shamba lenu. Au mgomba ule unaweza kuwa mali ya jamaa

nyingi na wote wameruhusiwa kula ndizi zake. Je! ikiwa mgomba huu uko katika shamba la mtu mwingine utafanyaje? Je! ni vizuri kwenda na kuchukua ndizi zake? La, hashu,



hadi kwanza utakapomwuliza mwenyewe naye akuruhusu kuchukua ndizi zake.

Wakati mwingine unaweza kujaribiwa kufikiri kwamba, "Nina mali chache sana. Mimi ni maskini. Mtu yule ni tajiri. Ana mali nyingi. Ni vizuri kwangu kuchukua tu sehemu ndogo." Si vizuri kufikiria hivi.

Haidhuru kiasi cha mali uliyonayo, bado kutakuwa na yule ambaye atakuwa na nyingi kuliko wewe. Jambo hili halikupi haki ya kumwibia mtu yule. Tunajua kwamba Mungu hataki kuona mtoto au mtu mwingine akiteseka kwa ajili ya njaa au mahitaji mengine. Hata hivyo, anatutaka tutumie njia inayofaa kwa kujipatia mahitaji yenu ya maisha.

ZAKAYO ANAACHA KUIBA



Tunasoma hadithi ya mtu aitwaye Zakayo katika Biblia. Zakayo alikuwa tajiri sana. Alitajirika kwa kutoza ushuru mwingi kuliko ilivyompasa. Alichukua zile pesa alizopata zaidi. Hali hakuwa na furaha. Aliweza tu kuwa na amani moyoni mwake baada tu ya kukutana na Yesu na kuamua kumpendeza yeye. Aliwapa wale watu aliowaiba mara nne zaidi ya mali yao alichokuwa. Alibaki sasa na pesa chache lakini akawa na amani na Mungu, ambayo ilikuwa bora zaidi. Soma Luka 19:1-10.

Waandishi hawakuiba pesa. Bali hawakuwa waaminifu katika kazi zao. Walitajirika sana huku wale wajane waliowasingizia kuwa wanawasaidia wakiendelea kuwa maskini. Waandishi hawa walitaka tu watu waseme kwamba wao walikuwa watu wazuri. Walitaka waambiwe kwamba wao walifuata vyema dini na ni watu wema. Yesu alisema kwamba, "Jihadharini na waandishi."

Wao husema maneno tofauti na hutenda tofauti. Soma yale ambayo Yesu alisema katika Marko 12:38-40.

KUDANGANYA NI WIZI

Je! kudanganya ni sawa na kuiba? Ndiyo! Unapodanganya na kuangalia kazi ya mwingine wakati wa mtihani huwa unaiba maarifa ya mtu mwingine na pia unaiba alama nyingi ambazo hungepata.

Kuna njia nyingi za kutotii amri hii isemayo, "Usiibe." Mfanya biashara anaweza kuwaibia wanunuzi wake wakati ambapo hawaambii bei kamili. Pengine atataka pesa za kilo mbili ya

nyama, hali amewapimia tu kilo moja na nusu. Mwanamke anayeua mboga anaweza kuweka zile zilizooza chini ndani ya gunia ili zisionekane. Hivyo ni kutokuwa mwaminifu na ni kuiba. Je! unapouza kitu huwa unasema bei kamili? Hapo kale wakati Amosi alipokuwa nabii, wafanya biashara hawakuwa waaminifu. Waliweka bei ili watoe pesa kidogo kuliko zile walizonunulia. Hii ilikuwa njia moja ya kuiba. Mungu hakuwafurahia kamwe. Soma Amosi 8:4-5.

Yesu akasema, “Mkinipenda, mtazishika amri zangu” (Yohana 14:15). Uaminifu ni njia iletayo furaha ya kweli. Ni lazima tuwe waaminifu kwetu wenyewe na kwa wenzetu. Hatupaswi tu kusema kwamba tunataka kumpendeza Mungu, bali tunapaswa kutenda kwa njia ionyeshayo kwamba tunataka kumpendeza Mungu. Njia moja ni kutii amri ya Mungu isemayo, “Usiibe.”

KAZI YA KUFANYA

Kuna watu wawili katika picha kwenye ukurasa huu. Andika jina la kila mmoja chini ya picha hiyo.

Je! yule mtu aliyesimama chini anamwambiaje yule aliyekaa mtini? Andika maneno yenyewe katika nafasi ifuatayo. Utayapata katika Luka 19:5.

Je! mtu yule aliyepanda mtini alifanyaje? (Luka 19:6)

Je! alikuwa na hatia ya dhambi ipi?

Alipotubu dhambi zake na kusamehewa alifanyaje? (Luka 19:8)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mahitaji” (Waefeso 4:28).

Ikiwa kweli tunamfuata Yesu, hatuwezi kuendelea kutokuwa waaminifu. Ikiwa tumeiba, ni lazima turudishe au tulipie kile tulichoiba. Ni lazima tufanye yaliyomema mbele ya Mungu na mwanadamu.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Kumi na Mbili


SEMA UKWELI KILA MARA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:16; Mathayo 12:33-37; Waefeso 4:15, 29-31

UONGO HUONDOA FURAHA

Amri ambayo tutajifunza leo inatwambia kwamba tusishuhudie uongo. Inasema kwamba, "Usimshuhudie jirani yako uongo." (Kutoka 20:16) Hii inamaanisha kwamba hatupaswi kusema maneno yasiyo ya kweli. Tunaweza kusema kwamba amri hii inamaanisha kuwa: Utapaswa kusema ukweli wakati wote na mahali po pote ulipo.

Uongo! Huondoa furaha kabisa! Uongo mmoja huzusha uongo mwingine. Mwishowe mtu hukuta amenaswa katika utando wa uongo aliosema. Tunapo washuhudia jirani zetu uongo huwa tumemdanganya mtu mwingine. Hatupaswi kusema uongo kuhusu mtu mwingine. Wala hatupaswi kumdanganya mtu




mwingine. Uongo unaweza kutuzuru sisi wenyewe na hata wenzetu. Uongo unaweza kuharibu sifa ya mtu mwingine. Uongo unaweza kuwafanya wenzetu wasituamini.

DHAMBI HUANZIA MOYONI

Yesu alikuwa akiangalia ndani ya moyo wa mtu alipokuwa akizungumzia kuhusu dhambi. Soma Mathayo 12:33-37.

Je! ni tunda lipi unalopata kwenye mti wa mwembe? Unapata maembe.

Je! ni nini kipatikanacho kwenye mti wa miba? Miba ndiyo hukua kwenye mti huo.



Je! ni nini kitokacho ndani ya moyo wako? Hiyo inategemea na aina ya moyo ulionao. "Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema, na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya" (Mathayo 12:35).

Hakuna ye yote kati yetu aliye na moyo mzuri. Kila mmoja amefanya dhambi. Yesu Kristo amemwaga damu yake ili tuweze kusafishwa na kutakaswa. Ni wakati tujapo tu kwake kwa imani na kumwomba atutakase ndipo tuwapo na moyo safi.

Mdomo ni sehemu muhimu ya mwanadamu. Mdomo husema yale ambayo tunafikiria miongoni mwa mwetu. Yesu akawaambia, "Maana kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake" (Mathayo 12:34).

Mdomo wa mtu yule ambaye moyo wake unajaa maovu husema maneno mabaya kama ya kulaani, uongo na kuzusha uvumi. Lakini moyo wa yule ampendaye Mungu na kutaka kumpendeza husema ukweli kwa njia ya upendo.

Kila Mkristo hujaribiwa kutumia vibaya mdomo wake. Paulo alitundikia mashauri fulani. Alisema kwamba tusitumie lugha mbaya, lakini tuseme tu maneno yale yaliyomema na yawezayo kuwasaidia wengine. Alisema pia tusiendeleo kuwa wachoyo na kukasirika haraka. Alisema kwamba tusiwepo na nafasi ya kugombana au kusema maneno makali miongoni mwa mwetu.

Hebu tujihadhari na yale tusemayo. Usiseme uongo. Uongo unaweza kuzusha tu shida. Watu hawawezi kuamini lo lote usemalo iwapo umezoea kusema uongo.



Njia ya Mungu inatutaka tuseme ukweli kwa moyo wa upendo. Hii ndio njia bora zaidi.

KAZI YA KUFANYA

Umeelewaje maana ya Maandiko yaliyoko katika somo lako?

Kuna sentensi katika upande wa kulia wa sehemu hii yanayozungumzia kuhusu Maandiko ya leo na ambayo halina neno moja. Chagua neno lifaalo kutoka kwenye orodha iliyoko upande wa kushoto.

- | | |
|--------|--|
| moyo | 1. Amri ya tisa inasema kuwa, "Usimshuhudie _____ yako uongo." |
| ukweli | 2. Yesu akawaambia, "Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazyao _____ wake." |
| jirani | 3. Paulo aliwaambia Wakristo wa Efeso kusema _____ kwa moyo wa upendo. |

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake..."
(Waefeso 4:25).

Kusema uongo juu ya wengine huzusha shida. Huleta uchungu moyoni. Maneno ya uongo yanaweza kuharibu sifa ya mtu mwingine.

Ikiwa sisi ni watu ambao hatuwambii ukweli jirani zetu, basi wao hawawezi wakatuumini.

Kusema uongo hutoka kwa moyo uliojaa uongo. Dhambi yo yote huanza katika moyo ambao haushirikiani na Mungu. Ikiwa mioyo yetu imejaa wema na upendo wa Mungu, itajazwa pia na upendo na wema kwa watu wengine.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA NNE

YESU NA SHERIA

J3 - 4Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Kumi na Tatu

HATUPASWI KUWA WACHOYO

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:17; Luka 12:13-21, 29-31

Je! umewahi kumwona rafiki yako na kitu na ukataka sana kiwe chako? Ikiwa ulifikiria hivyo, basi ulikitamani. Mungu anasema katika amri ya mwisho kwamba, "Usitamani nyumba ya jirani yako" (Kutoka 20:17).



Je! "Kutamani" inamaanisha nini? Inamaanisha kutaka sana kitu cha mtu mwingine hata huwezi kufikiria jambo lingine. Njia nyingine ya kuelezea neno "kutamani" ni kuwaza sana jinsi ya kupata kile ambacho huna na huwezi kamwe kukipata.

Lakini, ungefanyaje iwapo ulikuwa na kila kitu ulichokitaka. Je! ungekuwa mwenye furaha? Yesu akamwambia, "...uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo." Uzima ni muhimu kuliko mali nyingi.

Yesu alisimulia hadithi kuelezea maneno yake. Kulikuwepo na mkulima mmoja tajiri sana. Shamba lake lilikuwa limezaa sana. Mavuno yake yalikuwa mengi sana na hakuwa na ghala za kutosha kuyaweka.

"Nifanyeje?" akajiuliza. "Sina pa kuyaweka akiba mavuno yangu." Haikumchukua mkulima yule muda mwingi kujua jibu la tatizo lake. Angezivunja ghala zake zile ndogo na

ajenge zingine kubwa. Halafu angejiambia, "Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi" (Luka 12:19).



Hebu fikiria! Mtu huyu alikuwa tajiri sana hata hangewazia jinsi ya kupata pesa kwa miaka mingi ijayo. Alifikiria iliyobaki kwake ni kufurahia tu.

Kulikuwa na kosa moja katika maisha ya mtu huyu. Je! alikuwa amemsahau nani? Alimsahau Mungu! Hakumfikiria Mungu wala jinsi ya kumpendeza. Alikuwa amesahau kwamba, "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu" (Waebrania 9:27). Wakati huo aliowekewa ulimfikia mapema sana kuliko alivyofikiria. Ulimfikia usiku huo huo. Mtu yule alienda kulala wala hakuamka tena. Alikufa. Mungu alimwuliza swali rahisi sana, "Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya

nani?" (Luka 12:20). Mtu yule hakuja na mali yo yote ulimwenguni wala hangeenda na mali yo yote.

Si vibaya kuwa na mali. Si vibaya kuwa na baisikeli au kutaka kujinunulia moja. Lakini ni vibaya kufanya kitu cho chote au tamaa ya kitu cho chote kuwa kuu zaidi kuliko jinsi tunavyotamani kumtumikia Mungu.

Yesu alitwambia tuatafute kwanza ufalme wake na tutaongezewa vitu vingine tunavyohitaji. Na wewe je? Je! unautafuta kwanza ufalme wa Mungu?

KAZI YA KUFANYA

Aya ifuatayo ina habari za yule mkulima tajiri. Baadhi ya sentensi zake si sawa. Piga mstari chini ya sentensi yote ambayo ni ya kweli. Halafu soma sentensi yote uliyopiga mstari na uone kama yanasimulia hadithi iliyoko katika Luka 12:16-21.

Mkulima mmoja tajiri alikuwa na shida. Ghala zake zilikuwa ndogo sana. "Nifanyeje?" akawaza. Sina nafasi ya kutosha ya mavuno yangu. Halafu akawakumbuka wajane na mayatima waliomaskini. Akaamua kuwapatia chakula. Akajiwa na wazo: Nitavunja ghala zangu na nijenge zingine kubwa zaidi. Aliamua kuuza mavuno yale na kupatia kanisa pesa atakazopata. Alifikiria kwamba hana jambo lingine la kuwazia. Alikuwa na pesa nyingi. Kuanzia wakati huo,

alifikiria kwamba atakula, anywe na kufurahia tu. Mungu akamwambia, "Nimefurahi kwa sababu unafikiria pale ambapo utaishi milele." Mungu alimwita mtu huyu mpumbavu kwa sababu hakuwa na Mungu maishani mwake. Mtu huyu alikufa usiku huo huo. Mfikirie Mungu kwanza, naye atakutunza.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Angalieni, jilindeni na choyo"
(Luka 12:15a).**

Mungu hatutaki tutamani au tuwe wachoyo. Anatutaka tushiriki na wenzetu vile vizuri tulivyo navyo.

Je! unajua jinsi watu wengine hushika nyani? Hutoboa tundu kwenye buyu. Tundu hiyo huwa kiasi cha kumwezesha tu nyani yule apitishe mkono wake. Halafu hujaza njugu katika buyu hilo na kulifungia juu ya mti.

Nyani yule huingiza mkono wake katika tundu hilo na kuchukua njugu mkononi mwake. Sasa huwa hawezi kutoa mkono wake nje kwa sababu hataki kuachilia njugu zile. Yeye hukaa tu hapó hadi wale watu waliomtega warudipo na kumkamata.

Watu wenye tamaa wako kama nyani huyu. Hawawezi kuachilia kitu cho chote walichonacho. Wanataka kujiwekea akiba yote.

Hebu tuombe na tumwambie Mungu atusaidie tusiwe watu wenye tamaa, lakini tufurahie kushiriki na wenzetu vitu tulivyonavyo.

